# Nani amerudi?
## Utendaji katika Bunge na uwezekano wa Wabunge kuchaguliwa kwa mara nyingine





## Utangulizi

Kipindi cha miaka mitano cha Bunge la 9 la Tanzania kilimalizika Julai 16, 2010. Katika sherehe ya kuvunja Bunge Rais Jakaya Kikwete alitoa hotuba kwa muda wa masaa mawili kwa Wabunge, hotuba aliyoiita "Tukiahidi, Tunatimiza". Katika hotuba yake hiyo, Rais alitaja mafanikio ya Serikali yake. Mnamo Oktoba 31, 2010, Watanzania walichagua wawakilishi wao watakaowawakilisha katika Bunge la 10. Wakati walipopiga kura, wananchi walitarajiwa kuzingatia mafanikio ya Serikali, pamoja na kiwango cha ushiriki cha Wabunge hao waliowawakilisha katika kipindi kilichopita. Je, walifanya hivyo?

Kipimo kimojawapo ambacho wapiga kura wanaweza kutumia wanapomtathmini Mbunge ni kwa kiasi gani Mbunge huyo alishiriki katika shughuli za Bunge. Je, wapiga kura wanaweka mkazo wowote katika kiwango cha maswali ya msingi na ya nyongeza aliyouliza Mbunge wao au katika kiwango ambacho Mbunge huyo amechangia hoja akiwa Bungeni? Muhtasari huu unawasilisha mambo sita makuu kuhusu kiwango cha ushiriki wa Wabunge katika Bunge la 9 na kufanikiwa kwao kurudi tena katika Bunge la 10. Taarifa zinazowasilishwa katika muhtasari huu zimepatikana kutoka tovuti ya Bunge (www.bunge.go.tz) na pia zinaweza kupakuliwa kutoka www.uwazi.org.

Muhtasari huu unaonesha kwamba chini ya nusu ya Wabunge wa kuchaguliwa wamerudi tena Bungeni katika mwaka 2010 na kwamba ni theluthi moja tu ya Wabunge wa kuchaguliwa wa kawaida (yaani, Wabunge ambao si watumishi wenye nyadhifa za juu katika serikali) ndiyo waliofanikiwa kubaki na viti vyao tena katika Bunge. Muhtasari huu unaonesha kwamba Wabunge wa kuchaguliwa wa kawaida waliorudi Bungeni ni wale

Muhtasari huu umeandaliwa chini ya uangalizi wa Johannes Hoogeveen wa Uwazi iliyopo Twaweza-Hivos Tanzania.

Uwazi, S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: info@uwazi.org. Tofuti: www.uwazi.org
Umetolewa Machi, 2011.


waliokuwa na ushiriki mkubwa zaidi kuliko wale ambao hawakurudi. Vile vile, muhtasari unaonesha kwamba vyama vya siasa vyenye Wabunge wenye ushiriki mkubwa katika Bunge vilipata viti zaidi katika uchaguzi wa Oktoba 2010, wakati chama chenye Wabunge ambao hawakuwa na ushiriki mkubwa Bungeni kilipoteza viti. Kwa pamoja, mambo haya yanaashiria kuwa utendaji wa Wabunge ndani ya Bunge una umuhimu mkubwa kwa wapiga kura.

## Mambo sita makuu kuhusu Wabunge ambao hawakurudi Bungeni

### Jambo la 1: Chini ya nusu ya Wabunge wa kuchaguliwa wamerudi Bungeni baada ya uchaguzi wa 2010

Bunge la 9 lilikuwa na Wabunge wa kuchaguliwa 231. Kati yao, wabunge 100 wamerudi Bungeni baada ya uchaguzi wa Oktoba 2010, ambapo 131 (asilimia 57) hawakurudi. Wabunge 18 wanawake (asilimia 50) hawakurudi, wakati Wabunge wanaume 122 kati ya 213 (asilimia 57) hawakurudi, idadi inayoashiria uwezekano zaidi kidogo wa Wabunge wanaume kutorejea Bungeni ikilinganishwa na Wabunge wanawake.

**Kielelezo 1: Idadi ya Wabunge wa kuchaguliwa waliorudi Bungeni baada ya uchaguzi wa 2010**





**Chanzo cha data:** Tovuti ya Bunge.

### Jambo la 2: Wabunge mawaziri na watumishi wengine wenye nyadhifa za juu serikalini walikuwa na nafasi nzuri zaidi kurudi Bungeni

Wabunge waliokuwa mawaziri au watumishi wengine wenye nyadhifa za juu serikalini (kama vile, naibu spika, spika, mwanasheria mkuu wa serikali, na wakuu wa mikoa) walikuwa na nafasi nzuri zaidi ya kurudi Bungeni kuliko Wabunge wa kawaida. Kama Kielelezo 2 kinavyoonesha, asilimia 80 (35 kati ya 44) ya Wabunge wa kuchaguliwa ambao walikuwa watumishi wenye nyahifa za juu serikalini walichaguliwa, ambapo asilimia 35 tu (65 kati ya 187) ya Wabunge wa kawaida walirudi Bungeni baada ya uchaguzi wa 2010.

**Kielelezo 2: Asilimia ya Wabunge wa kuchaguliwa waliorudi Bungeni, kwa nyadhifa zao Serikalini**





**Chanzo chadata:** Tovuti ya bunge.

## Jambo la 3: CUF na CCM vilikuwa na asilimia kubwa zaidi ya Wabunge ambao hawakurudi

Kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 3, asilimia 66 ya Wabunge wa kuchaguliwa wa kawaida wa CCM hawakurudi Bungeni baada uchaguzi, ambapo asillimia 67 ya Wabunge wa kuchaguliwa wa kawaida wa CUF hawakurudi Bungeni. Chama cha UDP ambacho Mbunge wake pekee alirudi Bungeni, na CHADEMA (asilimia 40) ndivyo vilivyokuwa na asilimia za chini zaidi za Wabunge wa kuchaguliwa wa kawaida ambao hawakurudi Bungeni baada ya uchaguzi 2010.

**Kielelezo 3: Asilimia za Wabunge wa kuchaguliwa wa kawaida ambao hawakurudi, kwa mujibu wa vyama**





**Chanzo cha data:** Tovuti ya Bunge.

### Jambo la 4: Wabunge wa kawaida ambao hawakurudi Bungeni walikuwa na ushiriki mdogo

Kati ya Wabunge wa kuchaguliwa wa kawaida 187 katika Bunge la 9, 65 wamerudi wakati 122 hawakurudi. Wastani wa michango iliyotolewa na Wabunge waliorudi ilikuwa juu kidogo kuliko ile iliyotolewa na Wabunge ambao hawakurudi. Kwa wastani, Wabunge waliorudi walitoa michango 92 katika kipindi chao cha miaka mitano, ambapo wale ambao hawakurudi kuwa na wastani wa michango 81.

**Kielelezo 4: Wastani wa michango katika Bunge la 9 iliyofanywa na Wabunge wa kawaida, kwa mujibu wa kurudi kwao Bungeni 2010**





**Chanzo cha data:** Tovuti ya Bunge.

### Jambo la 5: CUF ni chama pekee kilichorudisha Bungeni Wabunge wake wengi wenye ushiriki mkubwa

Jambo kuu la 4 linaonesha kuwa Wabunge waliorudi Bungeni walikuwa na ushiriki mkubwa. Iwapo mtu atatathmini kiwango cha ushiriki cha Wabunge waliorudi na wale ambao hawakurudi ki-chama, ataona kwamba ni CUF pekee ndiyo iliyorudisha Bungeni Wabunge wake wengi waliokuwa na ushiriki mkubwa. Wabunge 6 wa CUF waliorudi Bungeni walichangia hoja kwa wastani wa mara 116, ambapo wabunge 12 wa CUF ambao hawakurudi Bungeni walichangia hoja kwa wastani wa mara 72. Kwa upande mwingine, kwa CCM na CHADEMA hakuna tofauti kubwa katika idadi ya michango kati ya Wabunge waliorudi na wale ambao hawakurudi. Wabunge 55 wa CCM waliorudi walichangia hoja kwa wastani wa mara 83, ambapo Wabunge wa CCM 108 ambao hawakurudi walichangia kwa wastani wa mara 80. Wabunge 3 wa CHADEMA waliorudi walichangia hoja kwa wastani wa mara 174, ambapo wabunge 2 ambao hawakurudi walichangia hoja mara 173.

**Kielelezo 5: Michango katika Bunge la 9, kwa mujibu wa Wabunge waliorudi na wale ambao hawakurudi, ki-chama**




**Chanzo cha data:** Tovuti ya Bunge.

## Jambo la 6: Chama kilichokuwa na wabunge wenye ushiriki mdogo bungeni kilipoteza viti katika uchaguzi mkuu wa 2010

Chama kilichokuwa na Wabunge wenye ushiriki mkubwa katika Bunge la 9 kilifanikiwa kupata viti zaidi baada ya uchaguzi wa 2010. Kwa upande mwingine, chama kilichokuwa na wabunge wenye ushiriki mdogo kilipoteza viti. Jambo hili linaweza kuonekana katika Jedwali 1. Jedwali linaonesha kuwa Wabunge wa kawaida wa CHADEMA ndiyo waliokuwa na ushiriki mkubwa Bungeni (kwa wastani walichangia hoja mara 173). Wabunge wa CUF na CCM kwa kiasi fulani walikuwa na ushiriki mdogo ikiwa wale wa CUF walichangia mara 87 na Wabunge wa CCM walitoa michango 80.

Ili kutathmini iwapo idadi ya michango ilihusiana na matokeo ya uchaguzi, kolamu 3 na 4 katika Jedwali 1 zinaonesha asilimia ya Wabunge waliochaguliwa katika kila chama baada ya uchaguzi. (Jedwali 1 linawasilisha asilimia, na si idadi ya Wabunge kwa sababu idadi ya majimbo ya uchaguzi katika uchaguzi wa 2010 yaliongezeka kutoka 231 yaliyokuwepo katika uchaguzi uliofanyika 2005 hadi kufikia 239 katika 2010). Ukiangalia jedwali utaona kuwa chama kilichotoa michango mingi zaidi Bungeni (CHADEMA) kiliongeza asilimia yake ya Wabunge kwa zaidi ya mara nne, kutoka asilimia 2 hadi 9. Kwa upande mwingine, chama kilichokuwa na Wabunge wenye ushiriki mdogo zaidi (CCM), kilipunguza asilimia yake ya Wabunge Bungeni kwa asilimia 11 (kutoka asilimia 89 hadi asilimia 78). CUF, chama ambacho Wabunge wake walikuwa na ushiriki zaidi ya ule wa Wabunge wa CCM, kiliongeza kidogo asilimia yake ya Wabunge (kutoka asilimia 8 hadi asilimia 10). Matokeo haya yanaelekea kukubaliana na maoni kwamba wapiga kura wanazingatia kiwango cha ushiriki wa Wabunge wakiwa Bungeni wakati wanapoamua ni chama kipi wakipigie kura.

**Jedwali 1: Idadi ya michango kwa kila Mbunge na asilimia ya uwakilishi wa vyama katika Bunge**

| | Michango kwa kila Mbunge | Asilimia ya Wabunge katika Bunge la | Asilimia ya Wabunge Bungeni katika Bunge la 10 | Mabadiliko ya asilimia katika Wabunge baina ya 2005 na 2010 |
|---|---|---|---|---|
| **CHADEMA** | 173 | Asilimia 2 | Asilimia 9 | Asilimia +7 |
| **CUF** | 87 | Asilimia 8 | Asilimia 10 | Asilimia +2 |
| **CCM** | 80 | Asilimia 89 | Asilimia 78 | Asilimia -11 |
| **Vyama vingine (pamoja na UDP)** | NA | Asilimia 1 | Asilimia 3 | Asilimia +2 |
| **Wastani /jumla** | 85 | Asilimia 100 | Asilimia 100 | -- |

**Chanzo cha data:** Tovuti ya Bunge

## Hitimisho

Zaidi ya nusu ya Wabunge wa kuchaguliwa katika Bunge la 9 hawakurudi Bungeni baada ya uchaguzi wa Oktoba 2010. Wabunge ambao hawakuwa mawaziri au watumishi wenye nyadhifa za juu serikalini walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kutorudi Bungeni: ni asilimia 35 tu ya Wabunge wa kawaida ndiyo waliorudi Bungeni baada ya uchaguzi.

Katika muhtasari huu, tunaonesha kwamba katika Uchaguzi Mkuu wa 2010, wapiga kura walionekana kuzingatia kiwango cha ushiriki wa Wabunge katika Bunge la 9. Chama kilichokuwa na Wabunge wenye ushiriki mdogo Bungeni (CCM) kimepoteza viti vingi, ambapo chama kilichokuwa na Wabunge wenye ushiriki mkubwa Bungeni (CHADEMA) kimefanikiwa kupata viti zaidi.

Kidokezo kinachojitokeza katika matokeo haya kwa Bunge la 10 ni kwamba vyama vya siasa vyenye nia ya kukua katika siku zijazo vitahitaji kuwahimiza Wabunge wao kuwa washiriki wazuri katika shughuli za Bunge.

## Kiambatanisho 1: Idadi ya Michango iliyotolewa na Wabunge waliorudi na wale ambao hawakurudi (2010) kutoka Bunge la 9

| Jina la Mbunge | Jimbo la uchaguzi | Jinsia | Chama | Idadi ya michango | Wadhifa katika serikali | Nafasi baada ya uchaguzi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Abbas Zuberi Mtemvu | Temeke | Me | CCM | 25 | | Amerudi |
| Abdallah Salum Sumry | Mpanda Magharibi | Me | CCM | 7 | | Hakurudi |
| Abdisalaam Issa Khatib | Makunduchi | Me | CCM | 29 | | Hakurudi |
| Abdul Jabiri Marombwa | Kibiti | Me | CCM | 67 | | Amerudi |
| Abdulkarim Esmail Hassan Shah | Mafia | Me | CCM | 41 | | Amerudi |
| Adam Kighoma Ali Malima | Mkuranga | Me | CCM | 43 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Aggrey Deaisile Joshua Mwanri | Siha | Me | CCM | 68 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Ahmed Ally Salum | Solwa | Me | CCM | 44 | | Amerudi |
| Ahmed Mabkhut Shabiby | Gairo | Me | CCM | 26 | | Amerudi |
| Ali Ameir Mohamed | Donge | Me | CCM | 11 | | Hakurudi |
| Ali Juma Haji | Chaani | Me | CCM | 28 | | Amerdi |
| Ali Khamis Seif | Mkoani | Me | CUF | 76 | | Amerudi |
| Ali Said Salim | Ziwani | Me | CUF | 41 | | Hakurudi |
| Aloyce Bent Kimaro | Vunjo | Me | CCM | 133 | | Hakurudi |
| Amb. GetrudeIbengwe Mongella | Ukerewe | Ke | CCM | 80 | | Hakurudi |
| Amb. Abdi Hassan Mshangama | Lushoto | Me | CCM | 75 | | Hakurudi |
| Amb. Hamis Suedi Kagasheki | Bukoba Mjini | Me | CCM | 20 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Amb. Seif Ali Iddi | Kitope | Me | CCM | 8 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Ame Pandu Ame | Nungwi | Me | CCM | 35 | | Hakurudi |
| Ameir Ali Ameir | Fuoni | Me | CCM | 72 | | Hakurudi |
| Andrew John Chenge | Bariadi Magharibi | Me | CCM | 116 | | Amerudi |
| Anne Kilango Malecela | Same Mashariki | Ke | CCM | 92 | | Amerudi |
| Anne Semamba Makinda | Njombe Kusini | Ke | CCM | 682 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Athumani Saidi Janguo | Kisarawe | Me | CCM | 75 | | Hakurudi |
| Bakari Shamis Faki | Ole | Me | CUF | 72 | | Hakurudi |
| Basil Pesambili Mramba | Rombo | Me | CCM | 65 | | Hakurudi |
| Beatrice Matumbo Shellukindo | Kilindi | Ke | CCM | 72 | | Amerudi |
| Benedict Ngalama Ole-Nangoro | Kiteto | Me | CCM | 36 | | Amerudi |
| Benito William Malangalila | Mufindi Kusini | Me | CCM | 57 | | Hakurudi |
| Benson Mwailugula Mpesya | Mbeya Mjini | Me | CCM | 133 | | Hakurudi |
| Bernard Kamillius Membe | Mtama | Me | CCM | 49 | Waziri | Amerudi |
| Brg. Gen. Hassan Athumani Ngwilizi | Mlalo | Me | CCM | 46 | | Amerudi |
| Bujiku Philip Sakila | Kwimba | Me | CCM | 148 | | Hakurudi |
| Capt. George Huruma Mkuchika | Newala | Me | CCM | 58 | Waziri | Amerudi |
| Capt. John Damiano Komba | Mbinga Magharibi | Me | CCM | 76 | | Amerudi |
| Capt. John Zefania Chiligati | Manyoni Mashariki | Me | CCM | 90 | Waziri | Amerudi |
| Castor Raphael Ligallama | Kilombero | Me | CCM | 124 | | Hakurudi |
| Celina Ompeshi Kombani | Ulanga Mashariki | Ke | CCM | 34 | Waziri | Amerudi |

| Jina la Mbunge | Jimbo la uchaguzi | Jinsia | Chama | Idadi ya michango | Wadhifa katika serikali | Nafasi baada ya uchaguzi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Charles Muguta Kajege | Mwibara | Me | CCM | 62 | | Hakurudi |
| Charles Mwera Nyanguru | Tarime | Me | CHADEMA | 61 | | Hakurudi |
| Charles N. Keenja | Ubungo | Me | CCM | 95 | | Hakurudi |
| Christopher Kajoro Chiza | Buyungu | Me | CCM | 49 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Christopher Olonyokie Ole-Sendeka | Simanjiro | Me | CCM | 83 | | Amerudi |
| Clemence Beatus Lyamba | Mikumi | Me | CCM | 99 | | Hakurudi |
| Col. Saleh Ali Farrah | Raha Leo | Me | CCM | 15 | | Hakurudi |
| Damas Pascal Nakei | Babati Magharibi | Me | CCM | 67 | | Hakurudi |
| Daniel Nicodem Nsanzugwanko | Kasulu East | Me | CCM | 105 | | Hakurudi |
| Dr. Abdallah Omar Kigoda | Handeni | Me | CCM | 64 | | Amerudi |
| Dr. Ali Tarab Ali | Konde | Me | CUF | 89 | | Hakurudi |
| Dr. Anthony Mwandu Diallo | Ilemela | Me | CCM | 47 | | Hakurudi |
| Dr. Binilith Satano Mahenge | Makete | Me | CCM | 91 | | Amerudi |
| Dr. Charles Ogesa F. Mlingwa | Shinyanga Mjini | Me | CCM | 85 | | Hakurudi |
| Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya | Kwela | Me | CCM | 124 | | Hakurudi |
| Dr. Cyril August Chami | Moshi Vijijini | Me | CCM | 26 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Dr. David Mathayo David | Same Magharibi | Me | CCM | 25 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Dr. Diodorus Buberwa Kamala | Nkenge | Me | CCM | 42 | Waziri | Hakurudi |
| Dr. Emmanuel John Nchimbi | Songea Mjini | Me | CCM | 15 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Dr. Festus Bulugu Limbu | Magu | Me | CCM | 76 | | Amerudi |
| Dr. Guido Gorogolio Sigonda | Songwe | Me | CCM | 100 | | Hakurudi |
| Dr. Haji Mwita Haji | Muyuni | Me | CCM | 40 | | Hakurudi |
| Dr. Harrison George Mwakyembe | Kyela | Me | CCM | 93 | | Amerudi |
| Dr. Hussein Ali Mwinyi | Kwahani | Me | CCM | 34 | Waziri | Amerudi |
| Dr. Ibrahim Said Msabaha | Kibaha Vijijini | Me | CCM | 55 | | Hakurudi |
| Dr. James Alex Msekela | Tabora Kaskazini | Me | CCM | 19 | Mkuu wa Mkoa | Hakurudi |
| Dr. James Mnanka Wanyancha | Serengeti | Me | CCM | 38 | Naibu Waziri | Hakurudi |
| Dr. Juma Alifa Ngasongwa | Ulanga Magharibi | Me | CCM | 68 | | Hakurudi |
| Dr. Luka Jelas Siyame | Mbozi Magharibi | Me | CCM | 94 | | Hakurudi |
| Dr. Mary Michael Nagu | Hanang | Ke | CCM | 126 | Waziri | Amerudi |
| Dr. Milton Makongoro Mahanga | Ukonga | Me | CCM | 28 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Dr. Omari Mzeru Nibuka | Morogoro Mjini | Me | CCM | 53 | | Hakurudi |
| Dr. Raphael Masunga Chegeni | Busega | Me | CCM | 94 | | Hakurudi |
| Dr. Samson Ferdinand Mpanda | Kilwa Kaskazini | Me | CCM | 90 | | Hakurudi |
| Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa | Bagamoyo | Me | CCM | 119 | Waziri | Amerudi |
| Dr. Wilbrod Peter Slaa | Karatu | Me | CHADEMA | 284 | | Hakurudi |
| Dr. Zainab Amir Gama | Kibaha | Ke | CCM | 78 | | Hakurudi |
| Dr.John Pombe Joseph Magufuli | Biharamulo Mashariki | Me | CCM | 91 | Waziri | Amerudi |
| Dunstan Daniel Mkapa | Nanyumbu | Me | CCM | 58 | | Amerudi |
| Edward Ngoyai Lowassa | Monduli | Me | CCM | 23 | | Amerudi |

| Jina la Mbunge | Jimbo la uchaguzi | Jinsia | Chama | Idadi ya michango | Wadhifa katika serikali | Nafasi baada ya uchaguzi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Elisa David Mollel | Arumeru Magharibi | Me | CCM | 37 | | Hakurudi |
| Emmanuel Jumanne Luhahula | Bukombe | Me | CCM | 146 | | Hakurudi |
| Ephraim Nehemia Madeje | Dodoma Mjini | Me | CCM | 71 | | Hakurudi |
| Ernest Gakeya Mabina | Geita | Me | CCM | 78 | | Hakurudi |
| Estherina Julio Kilasi | Mbarali | Ke | CCM | 76 | | Hakurudi |
| Eustace Osler Katagira | Kyerwa | Me | CCM | 41 | | Amerudi |
| Ezekiel Magolyo Maige | Msalala | Me | CCM | 87 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Fatma Mussa Maghimbi | Chake Chake | Ke | CUF | 62 | | Hakurudi |
| Felix Christopher Mrema | Arusha | Me | CCM | 15 | | Hakurudi |
| Felix Ntibenda Kijiko | Muhambwe | Me | CCM | 114 | | Hakurudi |
| Feteh Saad Mgeni | Bumbwini | Me | CCM | 41 | | Hakurudi |
| Fred Mpendazoe Tungu | Kishapu | Me | CCM | 57 | | Hakurudi |
| Fuya Godwin Kimbita | Hai | Me | CCM | 125 | | Hakurudi |
| Gaudence Cassian Kayombo | Mbinga Mashariki | Ke | CCM | 71 | | Amerudi |
| George Boniface Simbachawene | Kibakwe | Me | CCM | 136 | | Amerudi |
| George Malima Lubeleje | Mpwapwa | Me | CCM | 233 | | Hakurudi |
| Gideon Asimulike Cheyo | Ileje | Me | CCM | 25 | | Hakurudi |
| Godfrey Weston Zambi | Mbozi Mashariki | Me | CCM | 265 | | Amerudi |
| Gosbert Begumisa Blandes | Karagwe | Me | CCM | 113 | | Amerudi |
| Hafidh Ali Tahir | Dimani | Me | CCM | 127 | | Hakurudi |
| Haji Juma Sereweji | Mwanakwerekwe | Me | CCM | 29 | | Amerudi |
| Hamad Rashid Mohamed | Wawi | Me | CUF | 180 | | Amerudi |
| Hamza Abdallah Mwenegoha | Morogoro Kusini | Me | CCM | 69 | | Hakurudi |
| Harith Bakari Mwapachu | Tanga | Me | CCM | 36 | | Hakurudi |
| Haroub Said Masoud | Koani | Me | CCM | 75 | | Hakurudi |
| Hasnain Gulamabbas Dewji | Kilwa Kusini | Me | CCM | 72 | | Hakurudi |
| Hassan Chande Kigwalilo | Liwale | Me | CCM | 89 | | Hakurudi |
| Hassan Rajab Khatib | Amani | Me | CCM | 6 | | Hakurudi |
| Hawa Abdulrahman Ghasia | Mtwara Vijijini | Ke | CCM | 74 | Waziri | Amerudi |
| Hemed Mohammed Hemed | Chonga | Me | CUF | 70 | | Hakurudi |
| Herbert James Mntangi | Muheza | Me | CCM | 138 | | Amerudi |
| Hezekiah Ndahani Chibulunje | Chilonwa | Me | CCM | 15 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Ibrahim Mohamed Sanya | Mji Mkongwe | Me | CUF | 61 | | Amerudi |
| Idd Mohamed Azzan | Kinondoni | Me | CCM | 64 | | Amerudi |
| Issa Kassim Issa | Mpendae | Me | CCM | 25 | | Hakurudi |
| Jackson Muvangila Makwetta | Njombe Kaskazini | Me | CCM | 80 | | Hakurudi |
| Jacob Dalali Shibiliti | Misungwi | Me | CCM | 112 | | Hakurudi |
| James Daudi Lembeli | Kahama | Me | CCM | 104 | | Amerudi |

| Jina la Mbunge | Jimbo la uchaguzi | Jinsia | Chama | Idadi ya michango | Wadhifa katika serikali | Nafasi baada ya uchaguzi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| James Philipo Musalika | Nyang'hwale | Me | CCM | 90 | | Hakurudi |
| Jenista Joakim Mhagama | Peramiho | Ke | CCM | 364 | | Amerudi |
| Jeremiah Solomon Sumari | Arumeru Mashariki | Me | CCM | 10 | Naibu Waziri | Amerudi |
| Job Yustino Ndugai | Kongwa | Me | CCM | 376 | | Amerudi |
| Joel Nkaya Bendera | Korogwe Mashariki | Me | CCM | 32 | Naibu Waziri | Hakurudi |
| John Magale Shibuda | Maswa | Me | CCM | 30 | | Amerudi |
| John Momose Cheyo | Bariadi Mashariki | Me | UDP | 209 | | Amerudi |
| John Paul Lwanji | Manyoni Magharibi | Me | CCM | 169 | | Amerudi |
| John Samwel Malecela | Mtera | Me | CCM | 64 | | Hakurudi |
| Joseph James Mungai | Mufindi Kaskazini | Me | CCM | 36 | | Hakurudi |
| Juma Abdallah Njwayo | Tandahimba | Me | CCM | 84 | | Amerudi |
| Juma Hassan Killimbah | Iramba Magharibi | Me | CCM | 226 | | Hakurudi |
| Juma Said Omar | Mtambwe | Me | CUF | 72 | | Hakurudi |
| Juma Suleiman N'hunga | Dole | Me | CCM | 6 | | Hakurudi |
| Kabwe Zuberi Zitto | Kigoma Kaskazini | Me | CHADEMA | 261 | | Amerudi |
| Kaika Saning'o Telele | Ngorongoro | Me | CCM | 74 | | Amerudi |
| Khalifa Suleiman Khalifa | Gando | Me | CUF | 116 | | Amerudi |
| Kheri Khatib Ameir | Matemwe | Me | CCM | 39 | | Amerudi |
| Kilontsi Muhama Mporogomyi | Kasulu Magharibi | Me | CCM | 46 | | Hakurudi |
| Laus Omar Mhina | Korogwe Vijijini | Me | CCM | 64 | | Hakurudi |
| Lawrence Kego Masha | Nyamagana | Me | CCM | 75 | Waziri | Hakurudi |
| Lazaro Samuel Nyalandu | Singida Nonerth | Me | CCM | 60 | | Amerudi |
| Lolesia Jeremiah Bukwimba | Busanda | Ke | CCM | 17 | | Amerudi |
| Lucas Lumambo Selelii | Nzega | Me | CCM | 160 | | Hakurudi |
| Ludovick John Mwananzila | Kalambo | Me | CCM | 80 | | Hakurudi |
| Luhaga Joelson Mpina | Kisesa | Me | CCM | 57 | | Amerudi |
| Manju Salum Omar Msambya | Kigoma South | Me | CCM | 79 | | Hakurudi |
| Masolwa Cosmas Masolwa | Bububu | Me | CCM | 99 | | Hakurudi |
| Masoud Abdallah Salim | Mtambile | Me | CUF | 74 | | Amerudi |
| Mathias Meinrad Chikawe | Nachingwea | Me | CCM | 52 | Waziri | Amerudi |
| Mbaruk Kassim Mwandoro | Mkinga | Me | CCM | 102 | | Hakurudi |
| Monica Ngezi Mbega | Iringa Mjini | Ke | CCM | 6 | Mkuu wa Mkoa | Hakurudi |
| Mganalzumbe Msindai | Iramba Mashariki | Me | CCM | 237 | | Hakurudi |
| Michael Lekule Laizer | Longido | Me | CCM | 168 | | Amerudi |
| Mizengo Kayanza Peter Pinda | Mpanda Mashariki | Me | CCM | 40 | Waziri Mkuu | Amerudi |
| Mohamed Ali Said | Mgogoni | Me | CCM | 23 | | Hakurudi |
| Mohamed Habib Juma Mnyaa | Mkanyageni | Me | CUF | 186 | | Amerudi |
| Mohamed Hamisi Missanga | SingidaKusini | Me | CCM | 123 | | Amerudi |
| Mohamed Rished Abdallah | Pangani | Me | CCM | 161 | | Hakurudi |

| Jina la Mbunge | Jimbo la uchaguzi | Jinsia | Chama | Idadi ya michango | Wadhifa katika serikali | Nafasi baada ya uchaguzi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mohamed Said Sinani | Mtwara Mjini | Me | CCM | 40 | | Hakurudi |
| Mohammed Abdi Abdulaziz | LindiMjini | Me | CCM | 13 | Mkuu wa Mkoa | Hakurudi |
| Mohammed Amour Chombon | Magomeni | Me | CCM | 32 | | Amerudi |
| Mohammed Gulam Dewji | Singida Mjini | Me | CCM | 10 | | Amerudi |
| Mohammed Rajab Soud | Jang'ombe | Me | CCM | 70 | | Amerudi |
| Mossy Suleiman Mussa | Mfenesini | Me | CCM | 75 | | Amerudi |
| Mtutura Abdallah Mtutura | Tunduru | Me | CCM | 68 | | Amerudi |
| Mudhihir Mohamed Mudhihir | Mchinga | Me | CCM | 49 | | Hakurudi |
| Muhammed Seif Khatib | Uzini | Me | CCM | 25 | Waziri | Amerudi |
| Mussa Azan Zungu | Ilala | Me | CCM | 117 | | Amerudi |
| Mustafa Haidi Mkulo | Kilosa | Me | CCM | 112 | Waziri | Amerudi |
| Mwadini Abbas Jecha | Wete | Me | CUF | 99 | | Hakurudi |
| Mwinchoum Abdulrahman Idd Msomi | Kigamboni | Me | CCM | 85 | | Hakurudi |
| Mzee Ngwali Zubeir | Mkwajuni | Me | CCM | 68 | | Hakurudi |
| Nazir Mustafa Karamagi | Bukoba Vijijini | Me | CCM | 43 | | Hakurudi |
| Nimrod Elirehema Mkono | Musoma Vijijini | Me | CCM | 21 | | Amerudi |
| Omar Ali Mzee | Kiwani | Me | CUF | 47 | | Hakurudi |
| Omar Shabani Kwaangw' | Babati Mashariki | Me | CCM | 121 | | Hakurudi |
| Omar Sheha Mussa | Chumbuni | Me | CCM | 7 | | Hakurudi |
| Omar Yussuf Mzee | Kiembesamaki | Me | CCM | 49 | Naibu Waziri | Hakurudi |
| Oscar Rwegasira Mukasa | Biharamulo Magharibi | Me | CCM | 20 | | Hakurudi |
| Parmukh Singh Hoogan | Kikwajuni | Me | CCM | 48 | | Hakurudi |
| Paschal Constantine Degera | Kondoa South | Me | CCM | 119 | | hakurudi |
| Paul Peter Kimiti | Sumbawanga Mjini | Me | CCM | 127 | | Hakurudi |
| Peter Joseph Serukamba | Kigoma Mjini | Me | CCM | 98 | | Hakurudi |
| Philemon Ndesamburo | Moshi Mjini | Me | CHADEMA | 62 | | Amerudi |
| Philip Sang'ka Marmo | Mbulu | Me | CCM | 109 | Waziri | Hakurudi |
| Ponsiano Damiano Nyami | Nkasi | Me | CCM | 112 | | Hakurudi |
| Prof. David Homeli Mwakyusa | Rungwe Magharibi | Me | CCM | 144 | Waziri | Amerudi |
| Prof. Feethan Philipo Banyikwa | Ngara | Me | CCM | 39 | | Hakurudi |
| Prof. Idris Ali Mtulia | Rufiji | Me | CCM | 105 | | Hakurud |
| Prof. Juma Athuman Kapuya | Urambo Magharibi | Me | CCM | 68 | Waziri | Amerudi |
| Prof. Jumanne Abdallah Maghembe | Mwanga | Me | CCM | 143 | Waziri | Amerudi |
| Prof. Mark James Mwandosya | Rungwe Mashariki | Me | CCM | 118 | Waziri | Amerudi |
| Prof. Peter Mahamudu Msolla | Kilolo | Me | CCM | 63 | Waziri | Amerudi |
| Prof. Philemon Mikol Sarungi | Rorya | Me | CCM | 73 | | Hakurudi |
| Prof. Raphael Benedict Mwalyosi | Ludewa | Me | CCM | 193 | | Hakurudi |
| Rajab Ahmad Juma | Tumbatu | Me | CCM | 26 | | Hakurudi |
| Ramadhani Athumani Maneno | Chalinze | Me | CCM | 71 | | Hakurudi |
| Raynald Alfons Mrope | Masasi | Me | CCM | 129 | | Hakurudi |

| Jina la Mbunge | Jimbo la uchaguzi | Jinsia | Chama | Idadi ya michango | Wadhifa katika serikali | Nafasi baada ya uchaguzi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Rev. Luckson Ndaga Mwanjale | Mbeya Vijijini | Me | CCM | 18 | | Amerudi |
| Richard Mganga Ndassa | Sumve | Me | CCM | 64 | | Amerudi |
| Rita Louise Mlaki | Kawe | Ke | CCM | 28 | | Hakurudi |
| Rostam Abdulrasul Aziz | Igunga | Me | CCM | 0 | | Amerudi |
| Ruth Blasio Msafiri | Muleba Kaskazini | Ke | CCM | 140 | | Hakurudi |
| Said Amour Arfi | Mpanda Kati | Me | CHADEMA | 199 | | Amerudi |
| Said Juma Nkumba | Sikonge | Me | CCM | 63 | | Amerudi |
| Salim Abdallah Khalfan | Tumbe | Me | CUF | 31 | | Hakurudi |
| Salim Hemed Khamis | Chambani | Me | CUF | 177 | | Hakurudi |
| Salim Yussuf Mohamed | Kojani | Me | CUF | 11 | | Hakurudi |
| Salum Khamis Salum | Meatu | Me | CCM | 4 | | Hakurudi |
| Sameer Ismail Lotto | Morogoro -Kusini -Mashariki | Me | CCM | 14 | | Hakurudi |
| Samuel John Sitta | Urambo Mashariki | Me | CCM | 829 | Spika | Amerudi |
| Samuel Mchele Chitalilo | Buchosa | Me | CCM | 21 | | Hakurudi |
| Shoka Khamis Juma | Micheweni | Me | CUF | 96 | | Hakurudi |
| Siraju Juma Kaboyonga | Tabora Mjini | Me | CCM | 200 | | Hakurudi |
| Stanley Jilaoneka Yono Kevela | Njombe Magharibi | Me | CCM | 112 | | Hakurudi |
| Stephen Jones Galinoma | Kalenga | Me | CCM | 81 | | Hakurudi |
| Stephen Masatu Wasira | Bunda | Me | CCM | 165 | Waziri | Amerudi |
| Suleiman Ahmed Saddiq | Mvomero | Me | CCM | 11 | | Hakurudi |
| Suleiman Omar Kumchaya | Lulindi | Me | CCM | 76 | | Hakurudi |
| Tatu Musa Ntimizi | Igalula | Ke | CCM | 44 | | Hakurudi |
| Teddy Louise Kasella-Bantu | Bukene | Ke | CCM | 86 | | Hakurudi |
| Ussi Ame Pandu | Mtoni | Me | CCM | 40 | | Hakurudi |
| Vedastusi Mathayo Manyinyi | Musoma Mjini | Me | CCM | 92 | | Amerudi |
| Victor Kilasile Mwambalaswa | Lupa | Me | CCM | 94 | | Amerudi |
| Vita Rashid Kawawa | Namtumbo | Me | CCM | 135 | | Amerudi |
| Vuai Abdallah Khamis | Magogoni | Me | CCM | 91 | | Hakurudi |
| William Hezekia Shellukindo | Bumbuli | Me | CCM | 207 | | Hakurudi |
| William Jonathan Kusila | Bahi | Me | CCM | 9 | | Amerudi |
| William Mganga Ngeleja | Sengerema | Me | CCM | 176 | Waziri | Amerudi |
| William Vangimembe Lukuvi | Isman | Me | CCM | 7 | Mkuu wa Mkoa | Amerudi |
| Wilson Mutagaywa Masilingi | Muleba South | Me | CCM | 75 | | Hakurudi |
| Yahya KassimIssa | Chwaka | Me | CCM | 70 | | Amerudi |
| Zabein Muhaji Mhita | Kondoa Kaskazini | Me | CCM | 18 | | Amerudi |
| Zubeir Ali Maulid | Kwamtipura | Me | CCM | 149 | | Hakurudi |

**Chanzo cha data:** Tovuti ya Bunge.